# Vuta N'kuvute

**Shafi Adam Shafi**

Mkuki na Nyota
DAR – ES – SALAAM



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

Cheti cha Ithibati

NA. 853

Jina la Chapisho: Vuta N'kuvute

Mwandishi: Shafi Adam Shafi

Mchapishaji: Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

ISBN: 9976 973 29 3

*Kitabu hiki kilidhinishwa na EMAC tarehe* 30 *Mwezi* 6 *Mwaka* 2007 *kwa kitabu cha* Kujisomea *kwa ajili ya Kidato cha* 5 & 6 *katika* **Shule za Sekondari** *nchini Tanzania kulingana na Muhtasiri wa mwaka 20*05

R. A. Mpama

*MWENYEKITI*
*EMAC*

SEAL

KIMECHAPISHWA NA
Mkuki na Nyota Publishers Ltd,
S.L.P. 4246, Dar es Salaam, Tanzania
www.mkukinanyota.com

© Adam Shafi Adam Shafi, 1999

Mchoro wa Jalada na Martin van der Spuy
Sanifu mpya na Mkuki Bgoya

Chapa na Sanifu mpya, 2014

9976 973 29 2 (ISBN-10)
978-9976-973-29-7 (ISBN-13)

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuhifadhi, kuchapisha kwa njia ya kielektroniki au mekaniki, kutoa vivuli, kurekodi au kubadili sehemu yeyote ya kitabu hiki kwa njia, namna au mfumo wowote bila idhini ya maandishi kutoka kwa mchapishaji Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

Tembelea tovuti yetu www.mkukinanyota.com kujua zaidi kuhusu vitabu vyetu na jinsi pa kuvipata. Vilevile utaweza kusoma habari na mahojiano ya waandishi pamoja na taarifa za matukio yote yanayohusu vitabu kwa ujumla. Unaweza pia kujiunga na jarida pepe letu ili uwe wa kwanza kupata taarifa za matoleo mapya zitakazotumwa moja kwa moja kwenye sanduku la barua pepe yako.

Vitabu vya Mkuki na Nyota vinasambazwa nje ya Afrika na African Books Collective.
www.africanbookscollective.com

# Yaliyomo


Sura ya Kwanza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1
Sura ya Pili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 15
Sura ya Tatu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 28
Sura ya Nne . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 37
Sura ya Tano . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 50
Sura ya Sita . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 61
Sura ya Saba . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 74
Sura ya Nane . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 85
Sura ya Tisa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 113
Sura ya Kumi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 123
Sura ya Kumi na Moja . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 135
Sura ya Kumi na Mbili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 153
Sura ya Kumi na Tatu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 168
Sura ya Kumi na Nne . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 177
Sura ya Kumi na Tano . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 187
Sura ya Kumi na Sita . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 196
Sura ya Kumi na Saba . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 219
Sura ya Kumi na Nane . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 234
Tamati . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 244

*Kitabu hiki natabaruk kwa baba yangu*
*Shafi Adam Hila*

# Sura ya Kwanza

Mara tu baada ya kuvunja ungo, Yasmin aliozwa mume. Alikuwa mume wa jamii yake ya Ithnashiria ambaye alikuwa akiishi jirani naye hapo Mtendeni.

Alikuwa ni mume asiyelingana naye hata kidogo. Si kwa umri wala tabia kwani wakati Yasmin ni kigoli wa miaka kukmi na tano tu, mumewe Bwana Raza alikuwa zee la miaka hamsini na mbili. Wakati Bwana Raza keshazeeka, Yasmin alikuwa mtoto mbichi asiyeelewa kitu chochote.

Kukubali kwake kuolewa ilikuwa ni kwa sababu ya kuwaridhi wazee wake tu. Yeye mwenyewe hakuona fahari ya kuolewa na mzee anayeweza kumzaa. Hakupenda kufuatana na mumewe pahala popote pale na hata ile siku inayotokea wakaenda senema, basi yeye huwa hapendi kukaa karibu naye.

Yasmin alikuwa na kijiuso kidogo cha mdawari mfano wa tungule na macho makubwa ambayo kila wakati yalionekana kama yanalengwa lengwa na machozi. Alikuwa na pua ndogo, nyembamba na chini ya pua hiyo ilipangana midomo miwili mizuri iliyokuwa haitulii kwa tabia yake ya kuchekacheka, huku akionyesha safu mbili za meno yake mazuri. Alikuwa na kichaka cha nywele nyeusi zilizokoza ambazo zilianguka kwa utulivu juu ya mabega yake. Alikuwa si mrefu lakini hakuwa mfupi wa kuchusha, na matege aliyokuwa nayo yalizidi kuutia haiba mwendo wake wakati anapotembea.

Yasmin hakupenda hata kidogo kuolewa na mume kama yule kwani yeye mwenyewe angelipenda sana kupata mume kijana kama yeye mwenyewe. Alipenda ampate mume ambaye yeyote angelimwona angelisema, “Kweli Yasmin kapata mume.” Alikuwa anatamani kupenda lakini hakumpata wa kumpenda. Yeye alitaka kijana wa makamu yake ambaye angelimwonyesha pendo na yeye angelimiminia pendo lote moyoni mwake.

Kama desturi ya Wahindi wengi Afrika Mashariki Bwana Raza alikuwa mfanyabiashara mashuhuri pale mtendeni. Alikuwa na duka kubwa la biashara ya rejareja. Kwa kuwa duka hilo lilikuwa barabarani, basi kutwa lilivamiwa na washitiri waliokuwa na haja mbalimbali. Mara huyu kataka kibao cha mchele, huyu kataka fungu la tungule, huyu kataka bizari ya nusu shilingi na kutwa Bwana Raza alikuwa na kazi ya kupigizana kelele na washitiri wake. Tokea kuolewa kwake, Yasmin alikuwa ndiye msaidizi mkubwa wa Bwana Raza katika kazi hiyo.

Kutokumpenda Bwana Raza pamoja na utumishi wa kutwa dukani pale kulimfanya Yasmin ayachukie maisha ya unyumba na mumewe. Alitamani kufa kuliko kujitolea mwili wake kwa bwana yule. Inapofika usiku yeye huwa amejichokea na hulala mara tu baada ya kukiweka kichwa chake juu ya mto.

Hata baada ya kulala, Yasmin alikuwa haipati ile raha ya usingizi kwani mara kwa mara alikuwa akishituliwa na sauti nene ya kukwaruza ya mumewe ikimwita toka ukumbini kumwuliza swali hili au lile..

"Yasmin! Leo Bi. Mashavu alileta vitumbua vingapi?" Bwana Raza aliuliza, ameshughulika anafanya hesabu ya biashara ya siku ile. Yasmin huwa hajali maswali hayo na huendelea na usingizi wake bukheri. Anapokuwa hapo Bwana Raza hushughulika kweli hataki mzaha hata kidogo na mara kwa mara Yasmin humsikia akikasirika na kugombana peke yake. Inapokuwa hivyo huwa amekwisha pata hasara ya kitu fulani. Malalamiko ya kupata hasara yalikuwa hayamwishi na hata siku moja hutamsikia akisema amepata faida. Hiyo ilikuwa ni siri aliyoijua yeye mwenyewe tu.

Anapokuwa katika kazi hiyo ya kufanya hesabu Bwana Raza huvuta biri moja baada ya moja na moshi wa biri hizo huhanikiza harufu yake mbaya nyumba nzima. Baada yakumaliza hesabu zake Raza hufululiza moja kwa moja mpaka kitandani ambapo humkuta Yasmin amelala fo fo fo.

Chumba cha Bwana Raza kilikuwa kimejaa makorokocho. Mifuko ya unga, mikungu ya ndizi, maboksi ya majani ya chai makopo ya maziwa. Kuta za chumba hicho zilikuwa zimepambwa na picha mbili tu, moja ni picha ya maandishi yaliyokuwa kwa nakshi ya Kiarabu majina ya Fatma, Ali, Hassan na Hussein. Picha ya pili ilikuwa ni ya farasi aliyebeba mkono ulioonyesha vidole vyote vitano. Mlikuwa na kiti kizuri cha msaji kilichochongwa kwa nakshi pembeni na miguuni. Bwana Raza alinunua kiti hicho Darajani kwenye mnada. Kwenye pembe nyingine ya chumba hicho mlikuwa na kiti cha marimba na juu yake palikuwa na rafu iliyogongomelewa kwa misumari ukutani. Kwenye rafu hiyo palitundikwa maguo machafu na kwenye kijiti cha mwisho cha rafu hiyo ilining'inia tasbihi ndogo.

Chumba hicho hakikuonyesha kuwa ni pahala pa mtu kupumzika. Palikuwa ni pahala pa kupitisha usiku tu, kuche, asubuhi ifike biashara iendelee kama kawaida. Anapoingia chumbani humo baada ya kumaliza shughuli zake Bwana Raza huwa hana mazungumzo tena. Ni kuvua nguo na kujitupa kitandani. Hapo hujigaragaza na kugeuka ubavu huu na huu.

Mara hulala kifudifudi au mara hunyanyuka ghafla na kuwasha taa akitafuta biri na kiberiti. Akisha vipata vitu hivyo huwasha biri yake na kuivuta nusu kiasi cha kukifukiza chumba kwa moshi wa biri na halafu hujilaza tena kitandani. Hapo tena humgeukia Yasmin na kuanza kumpapasa na kumtomasatomasa akimwita na kumwuliza, “Yasmin ushalala?” Yasmin huwa kalala kweli yupo mbali katika ndoto zake za kitoto. Bwana Raza humgeuza huku na huku na kumpapasa papasa na mara mojamoja Yasmin huzinduka na kulala tena hapo hapo.

Kama kawaida yake, ghafla Bwana Raza aliinuka na kuwasha taa. Alichukua kiberiti na kuchomoa biri moja kutoka katika mfuko wa shati alilotundika juu ya rafu. Aliwasha na kuanza kuikupua mikupuo mikubwa mikubwa na kuyajaza mapafu moshi tele. Aliutoa moshi wote mara moja kupitia puani na mdomoni na mara hii badala ya kuivuta nusu alimaliza yote. Moshi ulijaa chumba kizima na hata ukampalia Yasmin. Alikohoa mpaka akaamka lakini alilala tena hapo hapo na alipoweka kichwa tu Bwana Raza alizima taa na kulala huku akimkumbatia mkewe.

“Usinikere Bwana mimi nataka kulala.”

“Mbona unalala mapema? N’do kwanza saa mbili. Amka tuzungumze,” Bwana Raza alinguruma. Yasmin alipuuza akalala.

Bwana Raza aliamka tena akawasha taa. Alimwangalia mkewe na kuanza kuuchunguza uzuri wake. Huo ulikuwa ndiyo wakati wa pekee ambao Bwana Raza anapata wasaa wa kumwangalia. Bwana Raza alirudi tena kulala baada ya kuzima taa na mara hii alimgeuza Yasmin ikawa nyuso zao zinatazamana. Alipotaka kujigeuza, Yasmin alihisi mikwaruzo mikali ya visiki vya ndevu za Bwana Raza, ndevu ambazo leo ya nne hakupata nafasi ya kuzinyoa.

Alihisi mikunjo ya uso wake na alipovuta pumzi alivuta hewa iliyojaa kupuo la moshi wa biri. Yasmin aligeuza uso wake huku na huku kumkimbia mumewe kijanja na mara alilala tena.

Kwa Yasmin usiku haukuwa mrefu mara kulipambazuka asubuhi ikaingia, kazi ya kuuza duka inamsubiri kama kawaida. Shughuli anayokuwa nayo Bwana Raza usiku kucha yeye hana habari nayo, yapitayo usiku kucha humkuta yeye katika dunia nyingine kabisa, dunia ya usingizi. Bwana Raza hakuwa na raha ya kuwa na mke na Yasmin ya kuwa na mume. Maisha ya watu wawili hawa yalikuwa ya bahati nasibu na hakuna mmoja kati yao aliyekuwa na raha na hali hiyo ilimfanya Yasmin kuondokea na

tabia ya unyonge akiona kama dunia imemwonea kuozeshwa mume asiye makamo yake wala asiyemvutia hata kidogo.

Ijapokuwa Yasmin alitumia muda wake mwingi dukani, lakini alipata muda wa kupanga ushoga na jirani yake Mwajuma. Mwajuma likuwa ni msichana wa Kiafrika na tabia yake ya ucheshi na masihara ilimfanya Yasmin avunje miiko ya Kihindi ya kutoingiliana na Waafrika.

Si ajabu kwa Yasmin kuvutiwa naye kwani yeye alikuwa ni kuvutio cha mtaa. Watoto, vijana na vizee, kila mmoja alijua namna yake ya kuzungumza naye. Pale panapojiri mzaha, furaha na busara basi yeye anazo nyingi.

Alikuwa ni mwanamke wa makamo tu, hazidi miaka ishirini na tano lakini umbile lake la wembamba lilimfanya aonekane yuko chini ya umri huo. Alikuwa na kisauti kikali azungumzapo kila jirani hujua kwamba Mwajuma yupo.

Alikuwa na uso mwembamba uliochongoka sawasawa na macho remburembu yaliyowafanya wenzake wampe jina la utani macho ya urojo," kwa kuwa yalirembuka kiasi ambacho asingeweza kutofautisha wakati amelewa na pale asipolewa. Majirani wengine wakisema eti anakula kungumanga.

Alikuwa mrefu wa wastani na avaapo lile vazi lake alipendalo la kujifunga kanga moja kiunoni na nyingine kujitupia mabegani, huku nywele zake amezisuka vizuri nne kichwa, huwezi kupita ukamtazama mara moja. Kila alipopata nafasi, Yasmin hupenya na kumtembelea Mwajuma nyumbani kwake, na yeye alikuwa ni mtu wa pekee ambaye Yasmin alimhadithia dhiki anayoiona kuishi na mume zee kama lile.

Hivi leo Bwana Raza amemaliza hesabu zake mapema na kuingia chumbani. Alikaa juu ya kile kiti cha msaji na kuanza kuvuta biri zake bila ya kuzungumza na Yasmin ambaye alikuwa bado yu ngali macho. Alikuwa amejilaza chali kitandani akiangalia boriti za chumba kile kama kwamba anazihesabu. Alikuwa mbali katika mawazo akifikiri vipi ataweza kumwepuka mzee yule, lakini kila alipofikiri hakuweza kupata kisingizio chochote cha kumkataa mumewe.

Bwana Raza akiwa na kipande cha biri mdomoni alianza kusema, "Siku hizi biashara hakuna. Kila nikifanya hesabu naona hasara tupu. Yule tajiri wangu wa Kibaniani amekataa kunikopesha vitu kwa sababu sikumlipa pesa za vitu nilivyochukua mwezi uliopita. Madeni yamenizunguka sijui

nitafanya nini." Yasmin alimtazama macho tu hakuwa na la kumjibu kwani mambo ya biashara hayakuwa kichwani mwake aslan.

"Mimi siwezi kuendelea na biashara namna hii, lazima nikatafute pahala pengine nifungue duka," Bwana Raza aliendelea kulalamika huku kipande chake cha biri amekikamata mkononi kwa ncha za vidole. Yasmin aliyapuuza yote yale akageuza ubavu upande wa pili, mara usingizi ukamchukua. Alipozinduka asubuhi ilikuwa ishaingia, Bwana Raza kashughulika anafungua duka.

Haikupita mwezi Raza alimwandikia Mamdali, mjomba wake anayeishi Mombasa na kumweleza matatizo yake ya kibiashara. Mamdali ni mtu wa Unguja aliyekwenda huko Mombasa zamani. Alikuwa mtu mashuhuri huko na kwa ajili ya utu uzima wake alikuwa na madaraka makubwa katika jumuiya ya Ithnashiria Mombasa. Yeye ana duka la fahari hapo Salim Road na wafanyabiashara wengi walimjua mzee huyo. Alikuwa na itibari kubwa na kwake yeye haikuwa vigumu kupata mkopo wa hata shilingi laki moja kutoka kwa tajiri yeyote yule.

Mara tu baada ya kupata barua ya Raza, Mamdari alimjibu na kumshauri ahamie Mombasa akaanzishe biashara ya mboga mboga ambayo inatija kubwa huko.

Yasmin na mumewe walikuwa wamekaa ukumbini wanakula chakula cha mchana. Bwana Raza alikuwa anawaza atayaanzaje mazungumzo ya kuhamia Mombasa. Waliendelea kula kwa muda kidogo bila ya kusemezana halafu Bwana Raza alianza, "Mke wangu mimi naona bora tuhame Unguja,"

Yasmin alipigwa na mshangao hakujua yameanzaje hata yakaja ya kuhama Unguja. "Kwa nini?" aliuliza.

"Ala! Si nimekwambia kwamba biashara siku hizi haziendi vizuri."

"Tuhame Unguja twende wapi?"

"Mombasa."

"Tukafanye nini?"

"Kwani sikukwambia?"

"Kitu gani?"

"Kwamba mjomba amenijibu ile barua yangu."

"Aa, mimi hukuniambia."

"Ala! Basi labda nimesahau, mjomba amenijibu ile barua niliyompelekea na amenishauri kuhamia Mombasa nikafanye biashara ya mboga."

Yasmin aliinama chini akiwa na kipande cha chapatti mkononi.

“Unasemaje?” Bwana Raza aliuliza, akiwa na hamu ya kutaka kujua mkewe atasema nini. “Ah! Haya maisha tunaoishi mimi na wewe, mimi yashanitumbukia nyongo. Mimi nahisi bora unipeleke kwetu wakati utakapokwenda Mombasa,” Yasmin alijibu kwa sauti ya hofu huku bado kipande cha chapati amekikamata mkononi.

Yasmin alikuwa akimwogopa sana mumewe kwa sababu ya mafahamiano mazuri yaliyokuwepo baina ya Raza na wazee wa Yasmin. Alihisi kumkera mumewe ni sawa na kuwakera wazee wake, ingawa Yasmin hakupenda kabisa kuishi na Bwana Raza. Yeye alitamani amwache lakini hakuthubutu kumtamkia maneno hayo. Alimwomba mumewe amrejeshe nyumbani lakini alikataa kata kata.

Bwana Raza alianza kuandaa safari mpaka ikanoga. Pasipoti yake na ya mkewe zilikuwa tayari na lililobaki ilikuwa ni kumwariifu Yasmini siku ya safari tu. Alisubiri wakati unaofaa kumpa habari hiyo na hapakuwa na wakati mwingine wowote isipokuwa usiku.

Raza alikuwa keshavuta biri zake zimemtosha wamelaa yeye na mkewe. “Yasmin,” Bwana Raza aliita taratibu.

“Unasemaje Bwana?”

“Safari imeiva, tutaondoka kesho kutwa, safari itatuchukua siku nne kwa meli. Tutapitia Pemba na Tanga.”

“Sasa kwani vipi yale maneno niliyokwambia n’do hukuyatia maanani?”

“Maneno gani hayo?”

“Nilikwambia unipeleke nyumbani na wewe utanguliye mimi nitakufuata baadaye.”

“Wacha maneno yako, tutafuatana mimi na wewe!” Bwana Raza alisema, tena sasa kwa hamaki. Yasmin hakuthubutu kujibizana na mumewe kwani hii haikuwa desturi yake. Alinyamaza kimya. Haikupita muda, kama kawaida yake usingizi ulimchukua.

Siku ya pili duka la Bwana Raza halikufunguliwa na majirani walikuwa washapata minong’ono kwamba bwana Raza na mkewe wanahama. Siku hiyo kutwa Bwana Raza na mkewe walikuwa kazini wakifunga funga. Yalifungwa makapu makubwa makubwa na siku hiyo biri zilikuwa zinavutwa mfululizo, moja baada ya nyengine. Kazi ya kufunga ilimalizika saa moja usiku. Yasmin aliona bora amwombe ruhusa mumewe ili apate kwenda kumuaga mama yake hapo Kiponda. Ruhusa ilipatikana na Yasmin alioga na kubadili nguo haraka na muda si muda alianza safari yake.

Kiasi cha saa mbili usiku alimkuta mama yake amekaa juu ya kochi ukumbini. Kabla hakuwahi kumsalimu, Zenabhai alianza kumvurumishia mwanawe maneno kwa, Kiswahili chake kibovu kilichosababishwa na kujitenga kwake na Waswahili kwa muda mrefu.

"Mbona umekujisha saa hizi peke yako?"

"Nimekuja kukuaga ma."

"Unakwendesha cha wapi?"

"Kwani Bwana Raza hakukwambia ma."

"Kunambilisha nini?"

"Sisi tunakwenda Mombasa kufungua duka."

"Raza hakukujisha hapa mezi nzima sasa mimi nafikirisha yeye iko gonjwa."

"Ah! Yeye mzima lakini kazi nyingi."

Yasmin hakukaa muda mkubwa kwa mama yake na baada ya kuzungumza kwa muda mfupi aliondoka kwa safari ya kurejea kwake.

Alipokuwa njiani Yasmin aliwaza kwamba haitakuwa jambo la busara kuondoka bila ya kumuaga hata mtu mmoja mtaani, kwa hivyo kabla ya kufika kwake alipitia kwa shoga yake Mwajuma.

Ngo, ngo, ngo, aligonga mlango. "Hodi, hodi wenyewe mmo humu ndani?"

"Nani mwenzangu?" Sauti kali iliuliza kutoka ndani.

"Mimi," Yasmin alijibu.

Mara Mwajuma alifungua mlango akiwa na taa ya kandili mkononi. "Oh! Yasmin, mbona saa hizi? Kwema?"

"Hakuna lililozidi shoga yangu, ila nimekuja kukuaga tu."

"Umekuja kuniaga, pita ndani basi."

"Ah! Nna haraka, siwezi kupita ndani manake sikumwambia mume wangu kama nitapitia kwako, yeye anajua kwamba nimekwenda Kiponda kwa mama tu basi nikichelewa yatakuwa mengine kwani kama unavyoyajua, baba lenyewe lina wivu kama nini sijui."

"Haifai hivyo, hebu pita ndani angalau dakika mbili," Mwajuma alisisitiza.

"Ah! Babu we, unayajua maneno ya mume wangu tena akianza kusema hamalizi."

"Ah, shoga yangu we, hayo yasikushughulishe, hiyo ndiyo desturi ya wanaume wazee wanaoowa wanawake watoto wadogo, basi maneno yake usiyajali."

“Basi n’takaa kidogo.”

Mwajuma alimkaribisha Yasmin ukumbini. Aliipandisha utambi taa aliyokuwa nayo mkononi ili wapate kuonana vizuri. Alimwomba akae juu ya bao lililokuwepo ukumbini pale na yeye mwenyewe alivuta mkeka pembeni na kukaa.

‘Ehee! Hebu nieleze za wapi tena?” Mwajuma aliuliza akitabasamu, sauti ameishusha chini.

‘Nasafiri mimi na mume wangu, tunakwenda Mombasa.”

“Tena babu maneno hayo niliyasikia yakizungumzwa mtaani lakini mimi sikuamini hata kidogo.”

“He! Ama kweli duniani hakuna siri, hivyo majirani washayajua?” Yasmin aliuliza, amepigwa na mshangao.

Mwajuma aliondoka pale alipokuwa amekaa juu ya meka akakaa juu ya bao yeye na Yasmin. Alimsogelea karibu na kumwuliza kwa kumnong’oneza. “Ati nasikia hutaki kumfuata?”

“Ah! Mwajuma we, hata la kukwambia sina, lakini funika kombe…”

Yasmin alipoinua mkono na kuangalia saa yake alistuka, “Lo! Saa nne kasorobo! Mtume! Si maneno hayo nikifika nyumbani, kwa heri, inshalla tutaonana tukijaaliwa.”

“Haya kwa heri shoga, hata mimi nna safari. Hivi unavyoniona nilikuwa nakwenda kuoga, leo kuna dansa la kukata na shoka hapo Mpirani wapigaji wanatoka Dar.”

“Basi kama hatukuonana n’do kwa heri,” Yasmin aliaga kwa sauti ya unyonge.

“Ahsante shoga kwa kuja kuniaga, usinisahau kwa barua ukifika Mombasa.”

Yasmin aliondoka kwa haraka kuelekea kwake, wasiwasi umemjaa. Baada ya kukata vichochoro viwili vitatu alijikuta ameshafika. Alifungua mlango taratibu, alipoingia ukumbini alimkuta Bwana Raza amekaa juu ya kiti amevimba kama kiboko.

“Mbona umekawia?” Raza aliuliza kwa kelele, amehamaki, moshi wa biri aliyokuwa akiivuta unatokea puani na mdomoni wakati huo huo.

“Mazungumzo ya mama yalikuwa marefu na mimi ilibidi nikae nimsikilize tu. Unajua tena akianza kusema.”

Raza alipumua kwa nguvu kama mtu aliyetuliwa mzigo mzito, “haya basi saa zishakuwa nyingi twende zetu tukalale.”

Siku ya safari ilipofika, waliamshwa alfajiri na sauti kali ya muadhini wa Jamatini iliyokuzwa kwa kipaza sauti kilichoifanya isikike waziwazi mpaka Mtendeni na sehemu zote zilizopo kando kando ya mtaa huo. Yasmin aliandaa vipochopocho vilivyotayarishwa tokea jana usiku. Walikula na walipomaliza walianza kuvalia. Walipomaliza kuvalia walionekana kama n'do kwanza wanatoka kuoana kasoro ujana wa Bwana Raza. Hapo Raza alianza kumtania Yasmin, "Nilikwambia tutasafiri kwa meli lakini nilikuwa nikikudanganya tu, tunasafiri kwa ndege. Ushawahi kupanda ndege wewe?" Raza aliuliza, akitabasamu na kuonyesha mikunjano iliyomjaa usoni.

Yasmin hakumjibu kitu ila na yeye alibakia kutabasamu tu utasema kwamba anaifurahia kweli safari ile. Ilipofika saa nne na nusu za asubuhi wote walikuwa wameshughulika pamoja na wasafiri wengine ndani ya kiwanja cha ndege cha Zanzibar. Baada ya hekaheka ya kujadiliana na watumishi wa Idara ya Uhamiaji na askari wa forodha, waliingia ndani ya ndege. Muda si muda walikuwa wanaelea ndani ya hewa ya Unguja iliyokuwa ikipepea moja kwa moja kutoka baharini, wakiacha chini yao ufukwe uliotambaa na kukizunguka kisiwa kile huku ukiwa umepambika kwa minazi iliyokuwa ikiyumba kwa maringo hewani. Walikaa bega kwa bega ndani ya ndege na Bwana Raza alimpisha Yasmini upande wa dirishani ili apate kumwonyesha maajabu ya kusafiri kwa ndege.

Ijapokuwa Yasmin alipendezewa sana na mandhari aliyokuwa akiyaacha chini yake, lakini mara kwa mara starehe aliyokuwa akiipata kwa kuangalia mandhari yale ilikuwa ikiharibiwa na jiso la Bwana Raza lililokuwa likimsogelea ama kumwambia kitu au kumwonyesha kitu. Walipaa juu kwa juu na baada ya safari ndefu walisikia sauti ya muhudumu wa ndani ya ndege akiwaarifu kwamba wanakaribia kutua. Walianza kuukabili ufukwe wa bahari ya Mombasa na baada ya muda kidogo walitua kiwanja cha ndege cha Mombasa. Jinsi Mamdali alivyokuwa maarufu Mombasa, aliingia mpaka ndani ya jengo la kiwanja sehemu ambayo raia wengine hawaruhusiwi. Aliwapokea Yasmin na Bwana Raza kwa furaha na heshima na msisimko wa furaha ile ulifikia kiwango cha kulizana. Vauxhall kipya lilikuwa nje likiwasubiri na baada ya safari fupi waliingia ndani ya jiji la Mombasa.

Walipofika nyumbani kwa Mamdali waliikuta nyumba imeshatayarishwa kwa wageni, kila kitu kimepangwa vizuri ndani ya ukumbi wa nyumba ile uliokuwa umejaa kila aina ya mapambo ya nyumbani. Nyimbo za Kihindi zilikuwa zikibembeleza kutoka kwenye radiogram kubwa lililokuwepo

kwenye pembe moja ya ukuta wa ukumbi ule na vijukuu vya Mamdali viliingia na kutoka vikiwa vimeshikwa na umbea wa kuwaona wageni.

Wiki moja tu baada ya kufika Mombasa Bwana Raza alitengenezewa kila kitu na Mamdali. Lilifunguliwa duka kubwa la biashara ya mboga. Ilikuwa hapana mboga utakayoitaka dukani hapo ukaikosa. Mchicha, kabichi, karoti, koliflawa, njegere, kisamvu na aina ya mboga kadha wa kadha.

Bwana Raza alikodi nyumba nzuri na kuipamba kwa mapambo ya kila aina hata ikakurubia ile ya Mamdali na mara hii chumba chake kilipambwa vizuri tofauti kabisa na kile chumba cha nyumba yake ya Mtendeni kilichokuwa kimejaa kila aina ya makorokocho.

Nyumba yake ilikuwa katika ghorofa ya pili ya jingo kubwa la roshani tatu. Dirisha la upande wa mashariki ya ukumbi wa nyumba lilitazama njia ya Kilindini jinsi ilivyonyooka moja kwa moja kuelekea bandarini na lile la upande wa magharibi lilitazamana na dirisha la nyumba ya jirani. Nyumba za mitaa ule zilikuwa za kizamani zilizoshikana moja baada ya nyengine, na zile za uapnde mmoja zilitenganishwa na za upande mwengine na barabara nyembamba za lami zilizouzongazonga mtaa ule. Kuta nene za udongo, chokaa na mawe zilipunguza joto ndani ya nyumba zile, kwani ifikapo mchana na, jua linapowaka mji wa Mombasa nao huwaka ukawa joto mtindo mmoja, lakini "Mombasa kongwe" ilikuwa na afadhali.

Mtaani hapo ndipo Bwana Raza alipoanzia maisha yake mjini Mombasa, mchana yuko sokoni jioni yuko nyumbani. Lakini tofauti na alipokuwa Unguja ambako mkewe alikuwa humsaidia katika biashara ya kuchuuza pilipili na bizari, biashara ya kuuza mboga sokoni Mombasa ilikuwa ni kazi ya peke yake, na Yasmini akawa ni wa kubaki nyumbani tu.

Kwa kuwa Mombasa kongwe haukuwa mtaa wenye maduka, wakati wa mchana ulikuwa shwari na walio majumbani kila mmoja huwa kashughulika na lake.

Kazi ya kumsaidia Bwana Raza ingawaje ilikuwa ikimchosha lakini ilikuwa ikimchangamsha, lakini leo wiki ya pili Yasmin anajihisi amepwaya ndani ya nyumba amezongwa na upweke kila pembe, hana wa kuzungumza naye. Kutwa kuchungulia madirishani. Tumbuizo pekee alilokuwa nalo zilikuwa nyimbo za Kihindi alizosikiliza kutoka katika radiogram kubwa lililosambaa kwenye pembe ya ukumbi.

Lakini Yasmin hakutoshelezwa na kukaa akisikiliza waimbaji wakighani na kutetea, bali mara mojamoja husimama katikati ya ukumbi akacheza. Huuyumbisha mwili wake, akatikisa matiti na kurembusha macho yake.

Mikono huinyanyua na kuishusha, akijibenua na kujinyonganyonga mithili ya mkunga aogeleavyo kupitia mapangoni. Alijifananisha na mchezaji nachi stadi wa filamu yoyote ile ya Kihindi. Siku zote afanyapo vituko hivyo hudhani yu pekee, yuko mbali na macho ya kiumbe chochote kile ambayo labda yangemtazama akatahayari. Ni macho ya Bwana Raza tu ambayo hayamtahayarishi na siku ambayo Yasmin hufurahi, Bwana Raza huwa ndiye mtazamaji pekee wa tumbuizo kama hilo. Akimchezea, akijipakatisha mapajani na kumbusu mashavuni na hapo ndipo Bwana Raza anapohisi maisha Mombasa yamenoga, biashara inamwendea vizuri Yasmin anamchangamkia hana wasiwasi.

Jumapili ile kulikuwa kumepambazuka vizuri mbinguni kukiwa na wingu kubwa lililojitandaza likawa kama mwavuli uliofunika mji wa Mombasa usichomwe na jua. Bwana Raza alitoka mapema kukimbilia sokoni kwani siku ile ya wiki ndiyo Wazungu na wale wanaojiweza wanapofanya manunuzi ya mahitaji yao ya wiki nzima. Tofauti na makabwera ambao kwao Jumapili ni siku ya kupumzika na wengine kulala mpaka saa nne wakiyabembeleza maruirui ya pombe ya jana, kwa wafanyabiashara wa sokoni, Jumapili ndiyo siku ya kazi hasa. Siku ya kuchuma fedha.

Yasmin naye aliamka na furaha iliyokuwa ikiendela tokea jana walipokwenda senema na kutembea tembea madukani. Waliporudi walikuwa na furaha. Furaha ile iliendelezwa kwa kila namna ambayo mume na mke hufurahishana ndani ya nyumba.

Baada ya kunywa chai alijihisi nyumba imemwelemea amezungukwa tena na upweke, akaanza kuufukuza upweke ule kwa kusikiliza muziki. Akajiwa na shauku ya kucheza, akasimama katikati ya ukumbi akaaza kujipinda na kujipindua. Hakuwa na habari kwamba siku zote anapokuwa mchezoni kuna mshabiki ashki wa mchezo wake, anayemwangalia bila ya yeye mwenyewe kujua. Ile ilipomalizika, leo yule ashki aliamua kumpongeza, akampigia makofi na kumwambia, “Shabash.”

Alipogeuka kuangalia dirishani, dirisha la nyumba iliyotazamana na ya kwao, akamgundua msungo aliyekuwa akichungulia unyago aliokuwa akiucheza. Walitazamana lakini Yasmin hakuweza kuvumilia mtazamo wa kijana yule aliyekuwa na macho makali kama kurunzi. Alisindika dirisha, ikawa ndiyo mwisho wa mchezo kwa siku ile.

Hakutahayari kama alivyokuwa akifikiri ila aliona fahari kuwa ngoma yake imepata mtazamaji zaidi ya bwana Raza kwani hata mwenyewe baadhi ya wakati alikuwa hujiuliza, “Ngoma gani hii isiyokuwa na mtazamaji?

Hata ngoma ya giningi huwa na watazamaji!" Na kuanzia siku hiyo ikawa ni desturi, Bwana Raza akishatoka kwenda kuchuuza mboga, ukumbi wa nyumba yake huwa uwanja wa mchezo wa nachi, mchezaji Yasmin mtazamaji jirani yake. Alikuwa kijana barobaro mwenye umbo la wastani. Alikuwa na macho makali ya rangi ya hudhurungi na nywele ndefu za mseto wa kipilipili na singa. Chini ya pua yake yalitambaa masharubu machanga yaliyodhihirisha kwamba n'do kwanza anaingia katika baleghi. Nyusi zake zilizokoza weusi zilianzia kutoka katika pembe zote mbili za uso zikaja zikakutana chini ya kipaji. Alikuwa ametulia dirishani akimtazama mwanamke yule jinsi anavyojibahashua mbele yake.

Kichwa cha santuri kilikuwa kinateleza juu ya njia za mwisho za sahani, mwimbaji anahitimisha nyimbo yake na ilipomalizika Yasmini alitulia akamtazama yule kijana, naye akamwuliza, "Nani kakufundisha?"

"Mwenyewe," alijibu, akitikisa kichwa kuzirudisha nywele zake nyuma.

"Unaweza kuwa mchezaji mzuri wa chakacha, ushawahi kuiona ngoma hiyo?"

"Bado."

"Unataka kuiona?"

"Ndiyo."

"Jumamosi Ali Mkali atapiga Sarigoi, utakwenda?"

Yasmin akaegemea juu ya kizingiti cha dirisha wakakabiliana uso kwa uso anafikiri la kumjibu. Sasa hakuona haya tena ila ameingiwa na hamu ya kutaka kujua zaidi juu ya ngoma ya chakacha, ngoma ambayo sifa zake amezisikia siku nyingi na nyimbo zake nyingi amekwisha zisikia na nyengine kuzihifadhi. Kuna nyimbo kama "kijembe," "mgomba", "usiniseme," na nyingi nyengine ambazo haipiti siku mbili bila ya kuzisikia mara mbili au tatu redioni, naye anazipenda. Aliinama akainuka, akamtazama yule kijana. "Nitakujibu," alimwambia.

Azue uwongo gani kwa mumewe ili ampe ruhusa ya kutoka usiku wa Jumamosi. Bado yungali mgeni mjini Mombasa, si jirani wala muhisani, si mjomba wala shangazi, hana wa kumzulia angalau akapata kisingizio cha kuomba ruhusa.

Kijana yule amempa mtihani mkubwa, wala hakumwona siku ya pili na ya tatu. Aliendelea na mtindo wake uleule wa kucheza ukumbini lakini kila alipoangalia dirisha la jirani aliona patupu, dirisha limefungwa. Alizidisha sauti ya radiogram angalau kama jiraniye yuko mbali asikie ishara kwamba ngoma imeanza, lakini wapi! Siku ya nne, wiki.

Sasa Yasmin alihisi zaidi ya kukosa mtazamaji wa ngoma aichezayo kuna kitu kingine akikosacho. Anamkosa jirani, kijana kama yeye. Alikuwa kama aliyekuwa kizani akaona nuru ya kumpa matumaini lakini ghafla nuru ile ikafifia. Mawazo ya chakacha yakayeyuka kichwani mwake na zile nyimbo alizokuwa akizisikiliza zikawa siyo za kusikiliza huku akicheza bali za kumletea athari ya kumfikiri mtu aliye mbali naye. Jumamosi ikapeperuka kama kishada kilichokatika arijojo bila ya Yasmini ikukumbuka kwamba ile ilikuwa ndiyo siku aliyotaka kuipangia uongo ili aruhusiwe kutoka akamsikilize Ali Mkali.

Sasa alibaini kwamba kumbe hamu yake haikuwa chakacha bali yule kijana ambaye alihisi labda atampunguzia unyonge kwa ile kuwa karibu na kijana wa rika lake, angalau akapata ile raha ya kuwa karibu nae wakaongea, wakacheka, wakafurahi. Kutoweka kwa kijana yule kukakawa kama wimbi lililoipiga nyumba ya Bwana Raza likafagia furaha changa iliyoanza kuchipua ndani ya nyumba ile. Mpaka Bwana Raza mwenyewe alihisi kwamba ule uchangamfu aliokuwa nao mkewe wakati wapya ndani ya nyumba sasa umeanza kufifia, akashindwa kuvumilia kamwuliza," Mbona siku hizi nakuona hivyo?"

"Vipi?"

"Si hivyo ulivyo!"

"Niko vipi?"

"Naona siku hizi…"

Kabla hata Bwana Raza hakumaliza Yasmin aliyachupia maneno, "Siku hizi unaona nini?"

"Naona siku hizi huchangamki, hata nachi huchezi tena."

"Kwani umenioa niwe nikikuchezea nachi? Kama unataka kuchezewa nachi si wende senema! Una nini mtu mzima wewe?"

Ulikuwa usiku wa kawaida tu, Bwana Raza keshakoga amejifunga kanga kiunoni amekaa kitini mguu wake wa kulia ameutundika juu ya wa kushoto anautikisa tikisa, sigara senti iko mkononi imemkolea anaikupua mikupou mikubwa mikubwa.

Ilikuwa karibu imdondoke lakini aliibana vizuri kwa kidole chake cha shahada na kile cha katikati. Amekaa kinywa wazi kama aliyepigwa kofi la ghafla, ameuachilia moshi wa sigareti ukijizongoazongoa taratibu kutoka kinywani mwake ukatanda pale ukumbini. "Unasemaje?" aliuliza, moshi bado ukimtoka kinywani.

“Kwani hukusikia?” naye Yasmin aliuliza, amekaa kwa maringo juu ya kiti, ameshika tama akimtazama Raza bila ya wasiwasi, pua ameikunja, mdomo ameufidua, jeuri ya kitoto inamwenda ndani ya damu yake. Bwana Raza akaona sasa maji yamezidi unga, hajui la kulifanya, Yasmin amechachamaa, amekuja juu kama mtoto wa kifuu lakini naye akajikaza ikambidi aonyeshe urijali wake. ‘Siku hizi umekuwa huna adabu!”

“Zinauzwa wapi? Hebu kanionyeshe nikazinunue.”

Bila ya kujua anafanya nini, Bwana Raza aliinuka akakitupa kile kipande cha sigareti alichokuwa nacho mkononi kikiungua tu bila ya kuvutwa, akamkamata Yasmin mkono akamnyanyua.

“Niwache au nitapiga kelele kama unataka kuniua mpaka majirani wote watoke madirishani.”

“Wewe! Nimekuchukua kwenu hohehahe! Huna mbele wala nyuma unanuka umaskini leo umekuwa jeuri enh?”

“Nani? Mimi? Unani…”

Kabla hakumaliza aliyotaka kuyasema Yasmin alitandikwa kofi kubwa; vimurimuri kila rangi vikawa vinameremeta mbele ya macho yake. Nuru iliyojaa ukumbini pale ikatoweka mbele ya macho yake pakawa kiza kitupu. “Unani…” Hajawahi kumaliza akachapwa kofi la pili. Yasmin alianguka juu ya kochi kama mzigo anatweta kama mgonjwa wa pumu.

Bwana Raza akili hana kichaa hana, midomo inamtetemeka, maneno yamemkwama hayatoki kinywani. Alitaka kumnyanyua Yasmin pale alipoangukia lakini Yasmin alichomoka ghafla akakimbilia mlangoni akaufungua. Mbio.

Bwana Raza naye akamwandama, naye mbio nyuma yake akimlaani na kumtukana, ngazi akishuka mbili mbili, lakini kabla ya kufika ghorofa ya kwanza kanga aliyojifunga kiunoni ilifunguka ikamvuka akawa uchi kama alivyozaliwa. Sasa ikawa kashfa imezaa kashfa, akaona amwachilie mbali “mwana kharam yule.” Yasmin akapotea ndani ya jiji la Mombasa.

Alipotoka nje hakujua amepotelea wapi akabaki kuizunguka nyumba akiwa tumbo wazi, na kanga tu kiunoni. Angelitokea askari bila ya shaka yoyote angelimkamata kwa kumtuhumu mwizi. Siku ile ilipita. Ya pili ikayoyoma na zifuatazo zikapukutika moja baada ya nyengine, hakumtia Yasmin machoni ng’o akabaki kuumwa ndani kwa ndani.

# Sura ya Pili

Yasmin alifika Unguja kwa meli kiasi cha saa kumi na mbili na nusu za magharibi, jua lilikuwa linapotea upande wa magharibi na mbingu zilikuwa zimepambika kwa mawingu ya rangi ya dhahabu yaliyochanganyikana na rangi ya zambarau. Abiria wote walikuwa washateremka melini na kila mmoja alikwenda alikokwenda isipokuwa Yasmin ambaye alibakia nje ya mlango wa kuelekea gatini, amesimama, amepigwa na bumbuwazi hana zaidi isipokuwa kikapu alichokuwa nacho mkononi. Wachukuzi namba walimzonga kama nzi wanapouzongea mzoga, kila mmoja katika wachukuzi wale akitaka kujua mizigo ya Yasmin ilipo ili akamchukulie.

Yasmin hakushughulika na yeyote katika wachukuzi wale ila aliwaona kama wendawazimu tu. Mawazo yake yalikuwa mbali na pale kilipo kiwiliwili chake na alikuwa akiwaza na kujiuliza, "Nende wapi saa hizi?" Alijiuliza na kujishauri moyoni mwake, "Nende kwa mama? Nikenda kwa mama atanitukana asinibakishe. Nende kwa mjomba? Ah! Nikenda kwa mjomba anaweza kunifukuza kwa kashfa ikawa aibu mtaa mzima."

Yasmin alijiuliza masuali kem-kem lakini jawabu linalofaa hakuligundua ng'o. Alianza safari yake ya kutokea bandarini kidogo kidogo akiwa na kikapu chake mkononi lakini wapi alikokuwa akienda hata yeye mwenyewe hakujua. Madereva wa teksi walizirambaza gari zao chini ya miguu yake lakini kwa wakati ule rasilimali yote ya Yasmin ilikuwa shilingi tano na kupanda teksi ilikuwa ni hasara asiyoweza kuimiliki ijapokuwa alikuwa amechoka na njaa kali imemshika.

Alijikongoja mpaka senema ya Malindi. Alikwenda moja kwa moja mpaka "Passing Show." Alipinda mkono wa kulia na kutokezea kwa Amar Waga. Hapo tena aliingia ndani ya barabara nyembamba za mtaa wa Malindi mpaka akafika kwa Rasam na alipofika hapo alitamani kupumzika lakini baada ya kujishauri aliona bora aendelee na safari yake. Moja kwa moja aliendelea mpaka "Dagger Club" na baada ya hatua chache alifika mbele ya mlango wa nyumba ya mjomba wake. Alijishauri kwanza kabla ya kubisha hodi. Alipogonga mlango alifunguliwa na mke wa mjomba wake ambaye kwa sauti ya mshtuko iliyochanganyikana na mshangao aliita, "Yasmin."

"Mjomba yupo?" aliuliza Yasmin hata bila ya kusalimu.

"Hayupo, kenda Jamatini. Mbona ghafla? Habari za Mombasa?"

"Mbaya."

“Kwa nini?”

“Kwanza usiniulize maswali mengi, njaa imenishika tena nimechoka, kama kipo chakula nigaiye kwanza nile halafu tutazungumza.”

Yasmin alikaa juu ya kiti na kukiweka kikapu chake chini. Palepale mke wa mjomba wake aliingia jikoni na kuanza kukaangakaanga. Kinywa cha Yasmin kilivuja mate kwa harufu nzuri iliyokuwa ikitokea jikoni na alihisi kwamba baada ya muda mfupi atakula kikomo cha shibe yake.

Kabla ya karamu aliyokuwa akiandaliwa haikuwa tayari mlango ulingongwa na alipokwenda kufungua alimkuta mjomba amemsimamia mbele.

“Mbona upo hapa saa hizi? Umerudi lini? Mume wako yuko wapi?” Yasmin hakujua ajibu lipi katika maswali aliyoulizwa. Alinyamaza kimya kama mtu aliyepigwa na bumbuwazi.

“Nakuuliza mume wako yuko wapi?” aliuliza tena mjomba wa Yasmin.

“Yuko Mombasa, mimi nimerudi nimeshindwa kuishi naye.”

“Unasemaje? Umeshindwa kuishi na Raza?”

Mjomba wa Yasmin aliondoka pale mlangoni alipokuwa amesimama. Aliingia ukumbini na kukaa juu ya kiti. “Enhe, hebu nieleze vizuri.”

Yasmin aliinamisha uso chini hofu imemjaa, “Mjomba, kusema kweli thawabu, mimi nimeshindwa kuishi na Bwana Raza. Kwa hakika mimi sikumpenda wala sikumtaka. Nilikubali kuolewa naye kwa kukuridhini nyinyi wazee wangu tu.”

“Kama hukuweza kuishi na Raza basi na sisi hatuna pa kukuweka,” mjomba wake Yasmin alisema kwa kelele. Kelele zilikuwa kubwa mpaka majirani wakaanza kuchungulia madirishani. “Tena upesi tuondokee mbele ya macho yetu utafute pa kwenda. Toka!” alifoka mjomba.

Yasmin alisita kidogo na kumtazama mjomba wake, matone ya machozi yakianza kuteleza taratibu kutoka kwenye macho yake mazuri.

“Nakwambia toka! Nenda zako! Nenda kamtafute huyo unayempenda.”

“Niondoke nende wapi na hapa ndiyo kwetu?” alisema Yasmin kwa unyonge.

“Hapa palikuwa kwenu kabla hujaolewa. Sisi tulikupa mume ili tupungukiwe na mzigo. Sasa madhali umemkimbia mumeo, tafuta pa kwenda.”

Yasmin mabega yalimporomoka, asijue la kufanya. Alitoka nje taratibu na alipofika nje mjomba wake aliufunga mlango kwa nguvu huku akilaani na kutukana. Majirani walikwishajaa madirishani wanamwangalia Yasmin

akitoa na kikapu chake mkononi, amenywea kama aliyemwagiwa maji ya baridi. Aliwaza na kujiuliza, “Nende kwa mama?” alifikiri, “Aa, nikenda huko mambo yatakuwa mabaya zaidi.”

Aliendelea na safari yake mpaka Darajani na alipofika hapo alisita kidogo. Alitia mkono sidiriani na kuzichomoa shilingi tano alizokuwa amezifutika na kuzitazama, akiwaza ni chakula gani atakachoweza kupata kwa pesa zile. Alikwenda mpaka kwa mchoma muhogo akanunua wa shilingi mbili. Alijibanza pembeni na kuanza kuula, akiula huku akifikiri na machozi kutaka kumtoka, zamani alikuwa akila muhogo wa kuchoma kwa kuutamani tu, leo anaula kwa njaa. Aliula wote na kupangusa midomo.

Sasa alizidi kufikiri pa kwenda. Alihisi balaa limemfika na janga limemwangukia hajui la kufanya. Palepale ilimjia fikra, “Bora nende kwa Mwajuma, labda ataweza kunisaidia.” Alikwenda moja kwa moja mpaka kwa Mwajuma. Alipofika hapo aligonga mlango na sauti ya Mwajuma ilimjibu kumkaribisha. Mwajuma alipofungua mlango na kumwona Yasmin alishangaa na kuuliza, “Yalikuwaje shoga yangu?”

“Ah, mambo makubwa, hata sijui nikwambie nini.”

“Karibu jikoni basi tupike.” Mwajuma alimsogezea Yasmin mbuzi na kumkaribisha akae yeye mwenyewe akiendelea na mapishi.

“Enhe! Khabari za Mombasa?”

“Khabari shoga yangu mbaya. Maisha na Bwana Mkubwa yule yamenishinda. Sina raha sina starehe, mwisho nimeona bora nirejee kwetu kwa wazee wangu. Nimekwenda kwa mjomba nimetimuliwa kama mbuzi na kwa mama naogopa kwenda manake maneno yake nayajua.” Yasmin alisita kidogo na kupumua. “Sasa hata sijui la kulifanya usiku huu,” aliendelea huku akikiweka kikapu chake alichokuwa amekikumbatia. Alikihisi kizito ijapokuwa bidhaa zote zilizokuwemo ndani ya kikapu kile ilikuwa ni kanzu moja na nguo za ndani mbili tatu alizogawiwa na jirani yake kule Mombasa. Labda kilichozidi ni mswaki na dawa ya meno.

“Maskini shoga yangu. Sasa una shauri gani?” Mwajuma aliuliza kwa huruma za dhati.

“Sina shauri lolote, nimekuja kwako kukusikiliza utaniambia nini. Tafadhali nisitiri, nisitiri aibu yangu!”

Mwajuma alimtazama Yasmin akatikisa kichwa. “Basi karibu shoga, tutajibana hapa hivyohivyo, ijapokuwa kitanda chenyewe kimoja,” alimwambia na kumwongoza chumbani akipangusa mikono kwa kanga aliyokuwa amejifunga kifuani.

Yasmin alikaribishwa chumbani. Baada ya kuingia ndani tu alikaa juu ya kitanda na kupumua kwa nguvu kwa machofu aliyokuwa nayo na wasiwasi uliokuwa umeyatawala maisha yake wakati ule. Mwajuma alimwacha Yasmin akipumzika na haraka haraka alimaliza kupika. Baada ya muda mfupi aliandaa wali mzuri uliokolea nazi, mchuzi wa chukuchuku na mboga ya mtoriro kidogo. Ilikuwa ni bahati tu kuwa siku ile Mwajuma hakuwa na nyendo za usiku, na baada ya kula tu walilala. Yasmin alilala usingizi mzito kwa machofu aliyokuwa nayo. Labda alizindukana mara mojamoja tu kujikuna mbu au kunguni aliyemtafuna, lakini alipokuja kuzindukana hasa kulikuwa kushakucha. Huko jikoni alimsikia Mwajuma akihangaika kukosha vyombo alivyopikia jana usiku na huko nje alisikia mlio wa kinu kilichokuwa kikitwangwa na watu wawili.

Haukupita muda, chai ilikuwa tayari na walipokuwa wakinywa Mwajuma alionekana ana haraka. Baada ya kumaliza tu alililitafuta baibui lilipo. Alivaa baibui, akasimama mbele ya kioo kirefu kiliomo chumbani mwake. Alijipaka podari, akajiremba wanja machoni. Alizichana nywele zake fupi ambazo leo hakuzisuka na baadaye aligeuka na kumtazama mgeni wake. "Mimi natoka mara moja. Nafika hapo Mbuyuni kwa mshoni wangu kusikiliza kama kanzu yangu iko tayari, nitarudi saa hivi."

"Mimi utanikuta hapahapa ukirudi," Yasmin alisema kwa unyonge wenye kutia huruma.

Mwajuma alitoka na kumwacha Yasmin peke yake. Hapo tena Yasmin alikabiliwa na kimya tu. Sauti za pekee alizoweza kuzisikia zilikuwa labda zile za mwuza samaki au mwuza mboga wakitangaza biashara zao kwa kelele.

Kwa Yasmin kimya kile kilikuwa cha sauti tu, kwani kichwani mwake mlikuwa mmejaa mawazo yaliyokuwa yakisokotana na kumfanyia kelele ambazo mtu yeyote hakuweza kuzisikia ila yeye mwenyewe. Aliondoka juu ya kiti alichokuwa amekikalia na kulala kitandani. Kitanda kilikuwa kimetandikwa vizuri kwa shuka ya rangi ya waridi iliyofumwa maua katikati. Wakati akigaragara juu ya kitanda kile, aliuchukua mmoja wa mito miwili iliyovikwa foronya rangi moja na ya lile shuka na kuukumbatia halafu akajilaza kifudifudi. Hapo tena fikra zilianza kutembea kichwani mwake na kuaza kujiuliza vipi ataweza kuyakabili maisha ilhali yu peke yake na yeye bado yu ngali mtoto hata ubwabwa wa shingo bado haukomtoka. Alijiuliza vipi ataweza kujiendesha? Mpaka lini ataishi kwa Mwajuma, mtu aliyemjua kwa mazungumzo tu? Nini jamaa zake watasema

wakisikia anaishi Uswahilini na Waafrika. Almureadi fikra namna kwa namna zilikuwa zinaranda na kupigana vikumbo ndani ya kichwa chake.

Alipogeuka alikikabili kile kioo kirefu kilichotundikwa ukutani na kama kioo kile kilikuwa kikimtua, aliinuka na kukisogelea. Sasa mawazo yote aliyokuwa nayo yalipeperuka kwa muda na kuanza kujianglia kioni namna alivyoumbika. Alijitazama na kujitazama tena, halafu akachukua kitana kilichokuwepo juu ya meza ndogo iliyokuwemo chumbani mle akaanza kuchana nywele zake na kuzilazia nyuma. Alijiona akizichana namna ile hapendezi. Alizichana tena na kuzilazia pembeni. Aligeuka na kujitazama huku na huku na alipohisi hajajifaidi bado, alifunga mlango. Alisimama mbele ya kioo akavua kanzu na kubakia na nguo za ndani tu.

Alijishika kiunoni kwa mikono yake na kujitazama tena huku na huku. Alijigeuza nyuma na kujiangalia lakini aliona bado hajajifaidi. Alivua sidiria na kujiangalia matiti yake na kuyainuainua huku akiyachezea. Alijigeuza tena mbele na nyuma na mara kwa ghafla, kama mtu aliyesituliwa, aliondoka mbele ya kioo na kuvaa nguo zake kwa haraka. Alipomaliza alijitupa kitandani na kulala kifudifudi na mara machozi yalianza kumtoka.

Zilimjia fikra za kwamba mtoto mzuri kama alivyo, mwenye mwili mzuri kama ule, leo anaishi maisha ya dhiki na unyonge vipi atakosa kupendwa na kijana mwenzake aliye mzuri kama yeye, tena aliye Mhindi. Kijana ambaye angelifuatana naye wakatia ngosho njiani huku vijana wenzake wakimhusudu. Alijiuliza, “Vipi?” Alifikiri labda Bwana Raza amemtia kisirani au labda amekaa ndani sana hata vijana hawakuwahi kumjua. Lakini kabla hakupata majibu ya maswali aliyokuwa akijiuliza, zilirudi kichwani mwake fikra juu ya maisha yaliyomkabili. Aliendelea kufikiri mpaka fikra zikamwisha, usingizi ukamchukua, akalala.

Hivi sasa Yasmin alikabiliwa na maisha mapya kabisa, maisha ambayo hakupata kuishi kwani ijapokuwa alikuwa akiishi Ng’ambu, lakini alikuwa haishi king’ambu. Alijuana na jirani zake wa Mtendeni kwa kuja kwao dukani kwa Bwana Raza tu, zaidi hapana. Ilikuwa ni bahati nzuri tu kujuana na Mwajuma, na hii ni labda kwa sababu tabia zao zimelingana.

Mwajuma, ijapokuwa ni mtoto wa kimaskini, alikuwa na roho nzuri ya ajabu na roho nzuri yake ilichanganyika na ukarimu usiokuwa na mfano. Alikuwa yuko tayari kumkirimu mtu chochote kidogo alichokuwa nacho. Alikuwa mwingi wa huruma na siku zote alikuwa tayari kumsaidia yeyote aliyemweleza shida zake, pindi akiwa na uwezo wa kumsaidia mtu huyo.

Kadhalika, alikuwa ni msichana asiyependa kujikera nafsi yake na aliutumilia uhuru wake wa maisha kama alivyopenda. Alikuwa tayari kufanya lolote lile ambalo alihisi litamletea furaha bila ya kujali wengine watasema nini. Kila Jumamosi alikuwa hakosi densini na alikuwa mpenzi mkubwa wa taarabu. Katika bahari ya muziki wa aina hiyo, alikuwa na sifa kubwa katika chama chake cha "Cheusi Dawa" kwa ajili ya sauti yake nyororo, kali wakati anapoimba. Asionyeshwe bi-harusi pahala popote pale, utamkuta Mwajuma amekwisha fika, amejitia kizoro pamoja na wasichana wenzake. Na hapo kwake, ingia toka ya vijana wa kike na wa kiume ilikuwa haishi. Yeye alikuwa hajali kusemwa na majirani ikiwa kwa wema au kwa ubaya, bali hufanya vile anavyopenda yeye mwenyewe.

Kiasi cha saa saba za mchana, Mwajuma alirejea kutoka safari yake ya randaranda mitaani na alimkuta Yasmin bado amelala. Ijapokuwa hakupenda kumwamsha, vishindo alivyovifanya wakati akibadili nguo vilimwamsha.

"Nimekukatia usingizi wako?" Mwajuma aliuliza, akihisi amemkera Yasmin.

"Ah, tokea hapo nilikuwa sina haja ya kulala, lakini usingizi umeniiba tu, "Yasmin alisema akijinyoosha. "Je usharudi safari yako?" aliuliza.

"Nimesharudi lakini yule mshoni sikumkuta. Nitakwenda kumsikiliza tena kesho."

Baada ya kubadili nguo, Mwajuma aliingia jikoni na kutayarisha mlo na alipomaliza walikula. Baada ya hapo alifanya kazi ndogondogo za kusafisha nyumba. Kisha ndipo likaanza gumzo baina yake na Yasmin.

"Mimi nilikuwa nikikuhisi kwamba humtaki Bwana Raza," Mwajuma alianza akiwa na hakika kwamba Yasmin atazungumza sana.

"Ah, yule alikuwa si mume wa kumtaka mimi mwenyewe niliozeshwa tu na wazee wangu na mimi sikuweza kuwavunja," alisema Yasmin akitabasamu na kuonyesha meno yake yaliyokuwa yaking'aa kama marmar.

Hapo tena liliendelea porojo baina ya Yasmin na Mwajuma kwa muda mrefu akizungumzwa Bwana Raza. Walimuumba na kumuumbua mzee huyo na mara mojamoja soga hilo lilistawishwa na hadithi za jiji la Mombasa. Hapo ulizungumzwa uzuri wa jiji hilo, jia pana la Kilindini lenye mataa mengi, maduka chungu nzima ya Mtaa wa Salim Road na harakati zinazokuwapo katika jia hilo usiku na mchana. Vitambaa na mapambo kila aina yaliyojaa ndani ya maduka yenye kupendeza. Na zinapoanza hadithi hizo ndipo Yasmin anapopata uwanja wa kuzungumza.

Aliyakumbuka mengi juu ya mji wa Mombasa, lakini katika kuhadithia kwake kote mwisho huangukia juu ya maisha yake na Bwana Raza na hapo soga juu ya Bwana Raza huendelea. Mwajuma na Yasmin walizungumza sana utafikiri hawakuonana kwa muda wa miaka kumi iliyopita. Ilipofika jioni wakati bado wamo katika starehe yao ya kupiga soga, waliingia vijana wawili. Walibisha hodi mara moja tu na hata kabla hawajawahi kujibiwa walijitoma ndani moja kwa moja mpaka chumbani kwa Mwajuma.

"Halo shem! Habari za kushinda?" aliuliza Salum, amesimama mlangoni mkono wake mmoja amekamata ubao wa mlango, mkono mwingine ameutia ndani ya mfuko wa suruali ya kaki aliyoivaa. Mwenzake amesimama karibu na pembe ya kitanda alichokalia Yasmin. Yasmin alikaa katikati ya kitanda amekumbatia mto mikononi mwake.

"He! Leo umepata mgeni wa Kihindi?" aliuliza Salum bado yungali amesimama mlangoni. Hakuonyesha heshima wala staha kwa mgeni yule ambaye hakupata kumwona hata siku moja.

"Aaaaa! Wacha maneno yako njoo ukae huku." Bila ya kuonyesha kwamba amekasirika au kuonyesha dalili yoyote ya furaha, Mwajuma alimkaribisha Salum kukaa juu ya kiti lakini badala ya kukaa pale alipokaribishwa alikwenda moja kwa moja mpaka kitandani na kujipweteka karibu na Yasmin.

Salum alimtumbulia macho Yasmin akaanza kumchungua tokea utosini hadi dole gumba halafu akamwuliza, "Hujambo dada?"

Yasmin alijibu kama aliyelazimishwa kusema akishangazwa na viroja vipya asivyopata kuviona. Aliondoka kwa haraka pale alipokuwa amekaa na kusogea mpaka pembe ya kitanda. Salum hakumshughulikia tena ila aligeuka upande wa pili na kumwangalia mgeni wake aliyemwandalia matembezi kwa Mwajuma siku ile.

"Roger pita ukae, usiwe na wasiwasi."

Halafu Salum alimgeukia Mwajuma na kumwambia, "Shem, huyu rafiki yangu kutoka Dar es Salaam. Tulikutana mwaka jana nilipokwenda huko kwa sherehe za Pasaka."

"Karibu Roger," Mwajuma alimkaribisha.

"Mbona mgeni wako kanikimbia?" Salum aliuliza akiingilia katikati ya mazungumzo ya kujuliana hali kati ya Roger na Mwajuma.

"Eh! Basi wewe umeingia kama shetani moja kwa moja mpaka kitandani na kuanza kumwangalia mtoto wa watu kama umeona ajabu gani sijui."

“Roger, pita ukae bwana,” Salum alimwambia rafiki yake aliyekuwa bado amesimama kwenye pembe nyingine ya kitanda amejawa na soni mbele ya wanawake wawili wale.

Roger alitabasamu huku akipita taratibu katikati ya chumba na kukaa juu ya kiti ambacho kilikuwa mbele ya kioo. Salum alimgeukia tena Yasmin akimtazama na kutabasamu akionyesha sura ya mtu asiyejali chochote. “Je, bibiye hujambo?” alimwuliza tena. Kwa sauti ya chini iliyochanganyikana na woga, haya na wasiwasi Yasmin alijibu, “Sijambo.”

“Mbona unaogopa dada; unafikiri si…”

Mwajuma alimkatiza maneno yake na kumwambia, “Hebu mwache huyo mtoto; unamtakia nini hasa? Na umetokea wapi saa hizi?”

“Nimetokea huko mtaani,” Salum alijibu, sasa ikawa ametulia amekaa katikati ya kitanda.

“Sasa vipi?” Mwajuma aliuliza.

“Namna gani?” Salum alitupa swali juu ya swali.

“Kaonane na yule mzee basi hapo nyuma.”

“Hilo ndilo lililonileta hapa,” Salum alisema na hapo hapo alisimama na kutia mkono mfukoni akatoa chungu ya mapeni yaliyochanganyika na funguo na pakiti ya sigareti iliyopondekapondeka. Alizihesabu zile pesa halafu akatikisa kichwa kukubaliana na hesabu yake na hapohapo alitoka bila ya kusema lolote. Baada ya Salum kutoka tu Mwajuma alianza kuandaa usiku wa siku ile. Alifungua kikabati kidogo kilichokuwepo karibu na alipokaa Roger ambaye alikuwa amekaa huku amepigwa na mshangao kwa mwenyeji wake kutoka bila ya kumweleza lolote.

Mwajuma alitoa gilasi nne kutoka kabatini mle na kuzitumbukiza moja ndani ya nyingine mpaka zikafanya mnara mdogo. Alikwenda nazo uani akiwaacha Roger na Yasmin peke yao ndani ya chumba. Walibakia chumbani mle kimya kama mabubu. Haikuchukua muda, Mwajuma alirudi na gilasi zake mkononi amekwisha zikosha vizuri na baada ya kukiondoa kitambaa kilichokuwa kimetandikwa juu ya meza alizipanga zile gilasi.

Kiasi cha Mwajuma kumaliza kuzipanga zile gilasi, aliingia Salum akiwa amefutika kitu kibindoni. Alisimama katikati ya chumba halafu akamtazama Roger. Alifungua kifungo cha shati na kuchomoa chupa ya rangi ya kijani iliyofungwa ki-stadi kwa kizibo cha jani kavu la mgomba. Aliinyanyua ile chupa juu, akiitikisa na mapovu makubwa yalitibuka ndani ya chupa ile, mapovu ambayo yalififia kila yalipopanda juu.

“Aha. mali safi hii, mali ya Mzee Kiroboto safi kabisa. Tofauti na wale wezi wanaouza maji matupu, unamaliza chupa nzima hata nishai hazikai sawa, lakini ya Mzee Kiroboto nusu tu,” Salum alieleza akikifungua kile kizibo cha chupa.

Kwa ghafla kile kizibo kilifunguka  na Salum alimwaga kidogo tende iliyokuwemo ndani ya chupa ile juu ya meza na kuiwasha kwa kiberiti. Palitokea mlipuko mdogo wa moto wa rangi ya kibuluu na moto ule uliunguza tende ile kidogokidogo mpaka ilipokauka na moto kuzimika.

“Unaona mambo hayo, mimekwambia mie kwamba mali ya Mzee Kiroboto peke yake,” alisifu Salum. Aliinua ile chupa akaanza kuimimina ile tende ndani ya gilasi zilizokuwa zimepangwa juu ya meza.

Kabla hakumaliza kazi ile Mwajuma alilalamika, “Ala! mbona hizo pegi unazitia kubwa? Umedhamiria nini leo?”

“Aaaa, Mwajuma we, unajifanya kama hujui desturi? Hujui kama pegi ya kwanza lazima iwe kubwa? Huyu mgeni wako vipi, nimtilie?” Salum aliuliza, ameikamata chupa mkononi tayari kumimina ndani ya gilasi iliyo karibu na Yasmin, “Ala! Nimesahau, Yasmin hanywi; au vipi utajaribu kidogo?” Mwajuma alimgeukia Yasmin na kumwuliza.

“Kwani kitu gani hicho?” Yasmin aliuliza amestaajabu.

Salum aliinama na kumwangalia Yasmin machoni na kumwuliza, “Bado hukujua nini hiki? Ulevi huu, utakunywa?” Yasmin hakujibu kitu ila aliinua mabega yake juu na kutikisa kichwa.

Salum alivunjika moyo na kusema kwa masikitiko, “Ooo, sikujua kama hunywi kimwana. Kwa nini usiniambie Mwajuma, nikamchukulia soda? Lakini haidhuru, tukimaliza chupa hii tutakwenda kuchukua nyingine na wakati huo nitapitia kwa Ashuru, nafikiri anazo soda baridi.”

Halafu Salum alimwangalia Mwajuma na kumwuliza, “Sasa shem, hakuna asusa yoyote ile?”

“Hakuna chochote,” Mwajuma alijibu.

“Basi katuletee maji, manake chuma hiki kikavukikavu hakipiti rohoni,” Salum alitoa shauri. Bila ya kupoteza wakati Mwajuma aliondoka na haikupita muda alirudi na kata iliyojaa maji.

“Haya tunywe, tunywe kwa afya ya mgeni wetu, Bibi Yasmin,” alisema Salum amenyanyua gilasi yake na kumwangalia Yasmin huku akitabasamu. Wote walinyanyua gilasi zao na kugugumia ulevi wote uliokuwemo ndani ya gilasi zile, kila mtu amekunja uso kama aliyekunywa shubiri. Na baada

ya hapo kata ya maji ilipelekwa duru na kila mmoja akagugumia mafunda mawili au matatu.

"Aaaa! Pombe ya Unguja safi kabisa, inashinda hata ile ya Darsalama," alisema Roger, akatikisa kichwa, uso bado ameukunnja hata baada ya kuzimua kwa maji.

"Unajua Bro, pombe kama hii lazima pawepo *'baiting'* japo kidogo, "Roger alitoa shauri lakini hapana yeyote aliyemjibu. Salum aliendelea kuzimimina pegi tu zikinywewa mojamoja, na kibao hicho kiliendelea mpaka ile chupa ikamalizika.

"Roger," Salum aliita, "Hebu nipeleke hapo kwa Mzee Kiroboto tukaongeze chupa nyingine, manake nahisi nishai bado hazijatulia kichwani, hazipandi wala hazishuki."

Bila ya kupinga au kujibu chochote, Roger kwanza alitoa paketi ya sigara akaizungusha duru na kila mvutaji alichuka moja. Halafu alitoa kiberiti, mwanzo alimwashia Mwajuma, halafu alimwashia Salum na mwisho aliiwasha sigara yake. Alivuta mikupuo miwili mikubwa moshi ukajaa ndani ya mapafu yake halafu akawa anautolea mdomoni taratibu akiviangalia viwingu vidogovidogo vilivyokuwa vikitoka mdomoni mwake. Baadaye aliondoka wakatoka yeye na Salum.

Walipokuwa njiani Salum alimshauri Roger, "Sisi tutakunywa robo-robo hukohuko kwa Mzee Kiroboto, halafu tutachukua chupa moja, lakini kwanza tutapitia dukani tukamchukulie yule mtoto mzuri soda na nafikiri hapohapo tutapata asusa."

Waliingia vichochoroni, Salum mbele Roger nyuma anafuata tu kama mkia. Kila njia aliyoiongoza Salum, Roger alikuwa nyuma, kila kichochoro naye yumo tu, anafuata bila ya kujua anaongozwa wapi. Walipita uchochoroni na walipoumaliza uchochoro huo walitokezea mbele ya uwanja uliozungukwa na nyumba zilizojengwa kwa miti iliyotomewa matope na mawe. Mbele yao, mandhari yaliishia kwenye upenu wa makuti ulioteremshiwa kipaa kifupi na chini ya kipaa hicho palipangwa matunda. Matango, machungwa, machenza, vipande vya mabalungi, na ndani ya sinia moja iliyokuwa na maji ndani mlikuwemo vipande vya matango vilivyopangwa vizuri.

Palikuwepo pia mafungu ya mboga ya mchicha, nazi, ndizi mbichi na pembeni yamepangwa mafungu ya muhogo.

Salum alisita kidogo, na Roger naye, kama askari aliyepewa amri na mkubwa wake, alisimama. Salum aligeuka na kutazama mkono wa kulia

halafu akatazama mkono wa kushoto na pembeni aliona kikundi cha watu waliovalia maridadi kabisa. Kanzu nyeupe na vizibao na wengine wamejitupia kashda mabegani. Baadhi yao walivalia kofia za mguu wa suruali zilizofuliwa na kupigwa pasi vizuri. Kila mmoja katika watu wale alikuwa amepakata kitabu mapajani wamezama katika darsa. Mmoja wao alikuwa akisomesha na wengine wanamsikiliza kwa makini.

Salum alisikiliza kidogo darsa ile lakini hakuelewa chochote kile katika yalokuwa yakisomeshwa. Kwa Roger yale yalikuwa n'do mageni kabisa kwani yeye hakupata kuyaona. Roger alipigwa na mshangao kwani hakujua wanakwenda wapi. Alistahimili kufuata nyuma kama mkia lakini mwisho alishindwa ikabidi aulize, "Oha, mbona…" lakini kabla hakuwahi kumaliza swali lake Salum alisogea mbele na kuelekea kwenye duka la mboga. Hapo tena walianza kuongozana kama mwanzo, Salum mbele Roger nyuma.

Walikwenda mpaka pale penye upenu wa duka na kukaa juu ya bao lililokuwepo pale. Roger alibakia kustaajabu, amesimama. "Kaa kitako," Salum alimwamuru.

"Mbona sioni mtu Bro?"

"Wewe kaa tu," Salum aliamrisha tena.

Roger alikaa juu ya bao kama alivyoambiwa na Salum lakini kabla hata hajakaa vizuri mwenye duka alitokea. Alikuwa mtu wa makamo, amevaa fulana isiyokuwa na mikono, miguu chini. Alipofika Salum alianza kuuliza bei ya ndizi mbivu, bei ya chenza halafu akauliza pombe kama ipo. Waliagiza robo robo wakaibugia mara moja na baadaye walianza kutafuna vipande vya matango kuutuliza ukali wa pombe ile.

Roger alitoa paketi ya sigareti, akachomoa sigareti moja na nyingine akamkaribisha Salum. Wote waliwasha sigareti wakawa wanazikupua harakaharaka. Baada ya kiasi cha mikupuo mitatu, Salum alitulia na sigara yake mkononi akisikiliza pombe inamwambia nini kichwani mwake. Alitulia kimya akili yake iko kule kunakosomeshwa darsa na darsa ile ilimvutia akisikiliza juu ya sheria za urithi za Kiislamu. Akifa baba, mtoto apate ngapi, mjomba apate ngapi. Lakini ghafla aliipuuza ile darsa.

Kwanza alijihisi hahusiki, kwani baba yake kafa zamani na yeye hakuwa na chochote cha kurithi. "Mzee Kiroboto," Salum aliita. Mzee Kiroboto hakuwa mbali, na kawaida yake ilivyo yeye haitwi mara mbili kwani kila wakati masikio yake huwa kwa washtiri wake. Mara moja Mzee Kiroboto alifika pale alipoitwa na iliagizwa chupa moja kama ilivyopangwa. Kufumba na kufumbua chupa ya tende ililetwa. Salum naye hakukawia kuipokea na kuchomeka kibindoni huku akiificha kwa shati lake. Aliichomeka

kistadi na hakuna mtu ambaye angeliweza kugundua kwamba alificha kitu kibindoni.

Walipoondoka pale walikwenda zao mpaka kwa Ashuru. Walimkuta amezungukwa na watu waliokuwa wakihitaji vitu mbalimbali dukani pale. Ilipofika zamu yao walinunua soda mbili, samaki wa kukaanga kwa wingi na peremende kali. Roger naye alichomoa paketi yake ya sigareti na kuiangalia. Alipoona sigareti zimebakia kidogo, alinunua paketi nyingine nahapo safari ilianza, tena mara hii kwa haraka zaidi kwa kuhofu wasije wakakamatwa na tende. Walipofika walimkuta Mwajuma anawasubiri kwa hamu kubwa kwani alikuwa amekwishachoka kujibu maswali kadha wa kadha aliyokuwa akiulizwa na Yasmin juu ya viroja vilivyokuwa vikitokea wakati wa karamu ile ya manywaji.

"Tumechelewa kidogo enh?" aliuliza Salum, jasho linamtiririka shati limefanya mabaka ya majasho kifuani. Alisimama mbele ya mlango na kupumua kidogo, halafu alifungua vifungo vya shati la mikono mirefu alilokuwa amevaa. Alifungua mlango na kulipachika pazia juu ili upepo mzuri uliokuwa ukitokea uani uwapitie na wao chumbani mle.

"Asusa hii," Salum aliweka furushi la samaki walofungwa ndani ya karatasi ya gazeti. Aliichomoa ile chupa kibindoni na kuiweka juu ya meza na halafu alitia mikono mfukoni mwake na kuchomoa chupa mbili za soda.

"Haya tuendelee na kibao," Salum alishauri. Alinyemelea kidogokidogo kitandani na kukaa palepale alipokuwa amekaa kwanza, karibu na Yasmin. Roger naye alinyemelea kidogokidogo akichelea asije akapepesuka na kuziangukia chupa zilizokuwepo juu ya meza. Kabla ya kukaa juu ya kiti alichomo paketi ya sigareti akaiweka juu ya mkono wa kiti halafu alikaa taratibu.

"Tukufungulie soda?" Salum alimwuliza Yasmin. Yasmin alibakia uso chini kwa haya nyingi zilizochanganyikana na kustaajabu. Aliinua macho na kumtazama Salum.

"Fungua hiyo soda Bwana!" amri ya ghafla ilitoka kwa Mwajuma. Salum hakujali amri iliyotoka kwa Mwajuma. Alipomwona Yasmin hakulijibu swali lake aliinuka na kuchomoa kutoka mfukoni mwake bunda la peremende kali. Alizitandika juu ya karatasi na kumkaribisha Yasmin kwa heshima kubwa. Alimgeukia Yasmin tena na kusema, "Chukua peremende basi ikiwa hutaki soda."

Sasa Yasmin badala ya kukasirika alitabasamu kwa mikasa aliyokuwa akifanya Salum. Alinyosha mkono na kuchukua peremende moja halafu akaitia mdomoni.

"Nmmm, wewe" Mwajuma aliguna akiichukua chupa moja ya soda. Alitoka nayo nje na aliporejea chupa ile ilikuwa ishafunguliwa. "Hebu Bwana Roger n'tolee gilasi moja humo ndani ya kabati," Mwajuma aliomba.

Roger alifungua kabati na kutoa gilasi moja ambayo alimkabidhi Mwajuma. Mwajuma aliimimina ile soda taratibu akichelea isije ikafoka. Alimpa Yasmin ile soda, naye kwa sauti ya chini alishukuru, "Ahsante."

Sasa ile chupa ya tende ilifunguliwa na pegi zikaanza kumiminwa kama kawaida. Baada ya pegi mbilimbili tu sauti zao zilianza kupaa na hasa ile ya Mwajuma. Zilipaa kidogokidogo kwa mazumngumzo namna kwa namna. Baada ya kiasi cha saa moja hii, hewa yote ndani ya chumba kile ilijaa moshi wa sigareti. Kelele zilizidi ikawa hawasikilizani tena, kila mmoja anazungumza lake.

Hapo tena Mwajuma jazba ilimpanda na kumjia hamu ya kutaka kuwatumbuiza wageni wake, na wageni wale walitumbuizwa kweli. Mwajuma aliimba nyimbo za kila mtindo, za taarabu, za unyago, chakacha na hata nyimbo za densi. Wakati Mwajuma alipokuwa katikati ya moja ya nyimbo zake, Salum aliyeonekana na nishai kubwa aliinuka kwa ghafla pale alipokuwa amekaa na kupiga kelele, "Ya salaam! Ukifa huozi mama!"

Roger alimtazama kwa jicho kali kama akitaka kumwambia, "Mbona unatukera katika starehe yetu?"

Baada ya hapo Salum alisimama na kukizunguka chumba, akicheza viuno kufuatishia nyimbo alizokuwa akiimba Mwajuma. Mwajuma aliendelea kuimba bila ya kujali vioja vya Salum. Chumba sasa kilikuwa kidogo mno ukilinganisha na tafrija zilizokuwemo mle. Salum naye katika kuufuatishia unsi ule, aligonga watu bila ya kujali na mara kwa mara aliisukuma ile meza iliyokuwa ikiandaliwa vinywaji. Katika zungukazunguka yake, alijistukia amesukuma na kuangukia juu ya kitanda pale alipokuwa amekaa karibu na Yasmin. Alipoinuka alimwona Roger amemsimamia mbele, ametoa macho kama chui anayetaka kulishambulia zizi la ng'ombe.

"Mbona unatukera, *Brother?* Unatuvunjia starehe yetu yote!"

Salum alijikusanyakusanya na kukaa vizuri, "*You fool!* Wewe unajifikiria nani hasa ndani ya nyumba hii?" Salum alipiga kelele akitaka kusimama, uso umemjaa shari. Mwajuma alinyamaza kuimba. Si uwanja wake tena. Sasa uwanja ni wa Roger na Salum.

“Sikilizeni, sitaki shari ndani ya nyumba yangu! Kama mnataka kupigana tokeni nje!”

Majirani waliojawa na umbeya walianza kutoka nje ya nyumba zao, wengine wamejitanda kanga, mwengine katoka na mtoto mkononi huku mtoto yule akilia, mwenye baiskeli mmoja alivunja safari yake na kutaka kujua kisa cha vurugu inayofanyika nyumbani mle.

“Wewe Roger siku zote unanisikia tu, lakini leo nitakuonyesha!” Salum alijinata. Alichupa na kutaka kumrukia Roger lakini alijistukia ameangukia meza na kuangusha chupa na gilasi zote.

Sasa sherehe iliyokuwemo chumbani mle iligeuka ugomvi. Yasmin alibakia ameshangaa akifikiri labda na yeye atapigwa kofi sasa hivi. Matumaini yake yote yalikuwa kwa Mwajuma, ambaye alikuwa na hakika atamnusuru pindi kikitokea chochote.

Mandhari kama yale hayakuwa mageni kwa Mwajuma, kwani kwa ugomvi tu, amekwishaona ugomvi wa kweli wacha vioja vile vilivyokuwa vikitokea chumbani mwake. Yeye aliokotaokota vitu na kuviweka vizuri, huku akimsihi Salum; “Babu kama umelewa nenda zako ukalale, usituvunjie starehe yetu. Mgeni umekuja naye mwenyewe kwa salama na amani; sasa umemgeukia unataka kumfanyia ubabe.”

Salum alijizoazoa na kusimama. Alipangusa shati lake lililokuwa limejaa mchanganyiko wa soda na tende iliyokuwepo juu ya meza aliyoiangukia.

“Salum naona siku hizi ulevi huuwezi. Bora uache. Kidogo tu mara ushakuwa unaanza shari. Bora acha! Tena tazama ulivyokukongoa, umebakia fremu tu,” Mwajuma aliendelea kumsimbulia.

Moyo wa Yasmin haukutulia mpaka alipomwona Salum amekaa. “Sasa n’do pombe yote imemwagika siyo?” aliuliza Salum kama kwamba hapakutokea chochote. *“Come on* Roger, twende tukachukue chupa nyingine.”

“Aka, kwa leo iwe basi,” aliamuru Mwajuma.

Tafrija ya siku ile ikaishia hapo. Salum na Roger wakatoka kama sio waliotaka kugombana sasa hivi.